



Novemba 19, 2021

Wapendwa Familia za PPS,

Ninatumaini kuwa kila kitu kiko sawa. Tumeamua kubadilisha Jumatatu, Novemba 29, kuwa siku ya kusomea nyumbani. Hii inamaanisha kuwa badala ya kuripoti shuleni Jumatatu, Novemba, wanafunzi wataingia mtandaoni wakiwa nyumbani na kukamilisha kazi zao wao wenyewe. Kama Mratibu wa Muda wa PPS, ninaamini kabisa ni kwa maslahi bora ya wanafunzi wetu, familia, wafanya kazi na jamii yetu kuwa niko mwaminifu kuhusu changamoto tunazokumbana nazo na ninaiweka wazi ni kwa nini maamuzi yanafanyika.

Uamuzi wa kubadilisha Jumatatu, Novemba 29, kutoka kuwa siku ya kusomea shuleni na kuwa siku ya kusomea nyumbani ulifanyika kwa sababu mbili.

1. Athari ya janga la COVID -19 inaendelea kuwoko katika maisha yetu ya kila siku. Kama vile katika tasnia nyingi, Wilaya yetu na wilaya za shule yetu, katika eneo na taifa nzima, tunapambana na upungufu wa wafanyakazi. Katika PPS, changamoto hizi za wafanyakazi zinazindishwa na kutokuwepo kwa sababu ya COVID, idadi chache ya wanaotuma ombi na ukosefu wa njia mbadala za kusoma.
2. Tumepokea ripoti kuwa tutakuwa na idadi chache ya waendeshaji basi na hivyo, tutakuwa na changamoto ya kuwapeleka wanafunzi shuleni.
3. Siku moja ya wanafunzi na wafanyakazi kufanya kazi wakiwa mbali inaipa timu yetu ya usimamizi siku ya ziada ya kuosha kabisa shule na vituo vyetu vyote, ikijumuisha wanyunyizi wa kielektrostatiki, kwa sababu ya kuongezeka kwa visa vilivyothibitishwa vya COVID-19 katika eneo hili.

Kuifanya siku ya kusomea nyumbani inaturuhusu kuihesabu siku hii kwa siku 182 zinazohitajika za masomo na kuondoa hitaji la kuongeza mwaka au kuondoa siku za likizo kutoka kwa Muda wa Mapumziko wa Majira ya Kuchipua. Kando na kukamilisha kazi, wanafunzi wataweza kufikia usaidizi wa Masomo na shughuli za Kijamii na Kihisia. Ili kuwekewa alama ya kuhudhuria, lazima wanafunzi waingie katika schoology katika wakati fulani mchana. Kila wakati, ikiwa mtoto wako atapata changamoto ya kuingia katika timu za Microsoft au Clever, tafadhali muarifu mwalimu wa mtoto wako. **wafanya kazi wetu waliojitolea wa Huduma ya Chakula watakuwa shuleni kutoa huduma ya chakula cha Kuchukua na Kwenda kutoka 1:00 Asubuhi to 7:00 mchana.**

Asante kwa usaidizi na uvumilivu wako huku ninapofanya kazi kukuza utamaduni unaoinua mafundisho na masomo bora kwa wanafunzi wote.

Wakati huu wa shukrani, ninakumbuka maneno ya mwandishi wa mashairi mumarekani, mwandishi wa kumbukumbu na mwanaharakati wa haki za raia Maya Angelou - "Kuwa katika mambo yote na ushukuru kwa kila jambo"

Ninaitakia familia yako likizo ya shukrani iliyo salama na ya kufurahia.

Wayne Walters, Ed.D.

Mratibu wa Muda wa Shule

Wayne Walters, Ed.D.  
Mratibu wa Muda wa Shule

341 S. Bellefield Avenue  
Pittsburgh, PA 15213

superintendentsoffice@pghschools.org  
Simu: 412-529-3600

Nambari ya Moja kwa  
Moja ya wazazi:  
412-529-HELP (4357)